Uwajibikaji na Usimamizi wa Maadili ya Asasi zisizokuwa za Kiserikali Tanzania

Sehemu ya 5 ya Sheria ya NGOs no.24 ya Mwaka 2002 inahusu la Uwajibikaji na Usimamizi wa Maadili kwa AZISE kuna vifungu namba 27 na 28 vinavyoagiza kuwepo Kanuni za Maadili kama Njia ya Kuhakikisha Uwajibikaji na Maadili bora ndani ya AZISE/AZAKI

Vifungu vya Sheria kuhusu Maadili

- 27.-(1) The Council shall develop and cause to be adopted a code of Code of conduct and such other regulations which shall facilitate self-regulation conduct of Non Governmental Organizations.
- (2) The Code of Conduct shall be adopted by a resolution at an annual Meeting of the Council.

Vifungu vya Sheria kuhusu Maadili

- 28.-(1) The Board shall have the duty to ensure that the code of conduct, regulations and rules developed by the Council are consistent with the national Policy for Non Governmental Organizations and the laws of the land.

- (2) The Board shall cause the code of conduct and regulations or rules developed by the Council to be published in the *Gazette.*

Mchakato wa Utengenezaji Kanuni za Maadili kwa AZISE/AZAKI Tanzania

- Mwaka 2005-Baraza la ASIZE (NaCoNGO) lilianzisha rasmi Mchakato wa Kuandaa Kanuni za Maadili
- Mwaka 2006-Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (The Legal and Human Rights Centre) Rasimu ya kwanza ya Kanuni za Maadili kwa kushirikiana na Tanzania Association of NGOs (TANGO) na kuikabidhi kwa NaCoNGO ambao walianza kushirikisha rasimu hiyo wadau mbalimbali kutafuta maoni

Mchakato …..

- Mikutano ya ushirikishwaji wa Rasimu au ya ukusanyaji maoni ilifanyika katika sehemu mbalimbali nchini kwa wadau kutoa Maoni yao (Mikutano ilifanyika Mtwara, Dodoma, Arusha, Iringa, Dar-es-Salaam-Tamasha la AZISE la TANGO (Viwanja vya Mnazi Mmoja) Tamasha la AZAKI la FCS la 2006 (Karimjee Hall), Mkutano wa AZAKI za Kimataifa zinazofanya kazi Nchini Machi 2006 (International NGOs Interest Group-IIG) na kwenye moja ya mikutano ya kila mwezi ya Policy Forum na wadau wengine mmoja mmoja waliochangia Maoni yao

Mchakato …..

- Mwaka 2007- Rasimu nyingine ya Kanuni za Maadili ilitengenezwa na Policy Forum kwa kushirikisha wadau wake mbalimbali kama Maoni yao jinsi Kanuni za Maadili ya AZISE/AZAKI ziweje.
- Mwaka 2007-Mwezi wa 9, FCS waliitisha mkutano wa wadau jijini Dar-es-Salaam kujadili hatua iliyofikiwa ya utengenezaji wa Kanuni hizo za Maadili na mwezi huo huo wa Septemba, uongozi wa Baraza (NaCoNGO) ulikutana na FCS na kukubaliana kukamilisha mchakato wa utengenezaji wa Kanuni za Maadili

Mchakato …..

- Mwaka 2007 –Octoba, Baraza lilikutana Morogoro na kupitisha rasmi Kanuni za Maadili ambazo zinatarajiwa kuwasilishwa bodi ya NGOs kwa hatua zaidi la urasimishaji wa Kanuni hizo.

- Bodi ya NGOs mpya ya NGOs imeundwa hivi karibuni na inatarajiwa kukutana hivi karibuni. Mojawapo ya masuala yatakayowasilishwa ni Kanuni hizi za NGOs.

- NaCoNGO inatambua kuwa Kanuni hizo hazijagusa kila kitu ambacho kila mdau angependa iwe bali ni kanuni za msingi (minimum principles) zitakazowawezesha AZISE/AZAKI kuthibitisha Uwajibikaji wao kwa wadau yaani wananchi/jamii, Serikali, Wafadhili na jumuiya ya wafanyabiashara (corporate sector). Nafasi ya kuzifanyia marekebisho ipo kwa kadri itakavyohitajiwa na AZISE/AZAKI zenyewe.

KANUNI ZA MAADILI

Lengo:

- Kuweka miongozo ya Uwajibikaji na Usimamizi wa Maadili ya AZISE/AZAKI nchini Tanzania. Kanuni hizi za Maadili zitatoa mwongozo kwa AZISE kufikia changamoto za uimarishaji wa Demokrasia, kuwa taasisi shirikishi na kuimarisha mazingira rafiki yatakayowawezesha wananchi, kwa pamoja au binafsi, kujiamulia hatima yao.

Madhumuni

- Kuimarisha na kushawishi kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika shughuli za AZISE/AZAKI nchini
- Kuchangia na kuimarisha misingi na taratibu za ufanyaji kazi wa AZISE/AZAKI nchini ili kuboresha uratibu na ushirikiano wa AZISE /AZAKI
- Kuimarisha mazingira ya ufanyaji kazi kwa AZISE/AZAKI.
- Kuweka taratibu zitakazohakikisha kuwa kanuni za maadili zinafuatwa na kutekelezwa na AZISE/AZAKI zote zitakazohusika na kanuni hizi.

MAENEO MAKUU YA KANUNI

- Utawala
- Uwajibikaji
- Usimamizi na Uwajibikaji wa Fedha
- Usimamizi wa Raslimali Watu
- Mawasiliano na Upeanaji taarifa
- Usimamizi na Utekelezaji wa Kanuni za Maadili

UTAWALA

- Tuhakikisha kunawepo kwa miundo ya Utawala iliyo wazi, yenye kazi na Majukumu wazi yanayoeleweka
- Tutahakikisha kunakuwepo kwa taratibu zilizowazi za kimaandishi kuhusu kazi, majukumu ya kiutawala kuhusu masuala kama mikutano, idadi ya Wajumbe, utoaji wa Taarifa n.k.
- Tutatengeneza na kufuata sera zinazohakikisha kutokuwepo kwa mgongano wa maslahi kati ya wanachama, viongozi, watendaji wakuu, watumishi na kazi za AZISE
- Tutahakikisha uongozi wa AZISE unachaguliwa au unateuliwa kwa kuzingatia misingi ya fursa sawa kwa wote na uwezo wa kila mtu
- Hatutavumilia na tutachukua hatua kwa aina zote za ufisadi (zero tolerance)

UWAJIBIKAJI

Tunatambua kuwepo kwa Uwajibikaji katika ngazi mbalimbali kwa mfano:

- Uwajibikaji kwa wananchi/jamii tunazozitumikia (downward accountability)
- Uwajibikaji ndani ya AZISE/AZAKI (internal accountability)
- Uwajibikaji kwa AZISE/AZAKI na wabia tunaofanya nao kazi (horizontal accountability)
- Uwajibikaji kwa Sera, Sheria na taratibu mbalimbali za nchi na za kimataifa (external accountability)

Uwajibikaji….

Ili kufanikisha haya;

- Tutahakikisha tunatoa taarifa kila wakati kuhusu dira, dhima, utawala na uongozi, taratibu za ufanyaji kazi na utekelezaji wa kazi za AZISE/AZAKI
- Tutatoa na kuhakikisha umma unapata taarifa za utekelezaji na fedha za kila mwaka kuhusu mafanikio, changamoto na mafunzo yaliyopatikana katika utekelezaji wa kazi za AZISE/AZAKI.

Sheria ya NGOs (Na. 24; 2002) inaagiza

- *29- (1) Each Non Governmental Organization shall for every*
- *(a) Prepare a report of its activities which shall be made available to the Public, the Council, the Board and other stake holders;*
- *(b) Prepare an annual audited report and submit copies thereof to the Council and the Board.*

Usimamizi na Uwajibikaji wa Fedha

- Tutatengeneza na kufuata taratibu zilizo wazi, za kueleweka za Usimamizi wa fedha ili kuthibitisha viwango vya hali ya juu ya Uwajibikaji.
- Tutahakikisha tunatumia gharama kidogo katika utafutaji wa fedha na katika Utawala na uendeshaji wa kila siku wa AZAKI
- Tutahakikisha Matumizi yanaidhinishwa kwa kufuata Utaratibu utakaowezesha watu zaidi ya mmoja wanahusishwa
- Tutahakikisha tunafuata taratibu za manunuzi zilizowazi, zinazokubalika na zisizotoa upendeleo wa aina yoyote
- Tutahakikisha taarifa zetu za fedha zinakaguliwa na wakaguzi huru wanaotambulika kisheria na tutatekeleza Mapendekezo ya wakaguzi hao.
- Hatutavumilia na tutachukua hatua kwa aina zote za ufisadi (zero tolerance)

USIMAMIZI WA RASLIMALI WATU

- Tunatambua na kuheshimu kwamba Asasi zinaundwa na watu ambao ni raslimali kubwa katika kufikia malengo ya kuanzishwa na kuwepo kwa Asasi husika.
- Tutahakikisha kuwepo kwa sera na taratibu zahaki na uwazi kuhusu raslimali
- Tutahakikisha na kuimarisha kuwepo kwa taratibu za wazi wa uajiri zinazotoa fursa sawa kwa wote na kwa kwa kuzingatia uwezo wa mtu
- Tutahakikisha taratibu za utafutaji watumishi na uajiri zinazingatia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa wataalamu wenyeji pasipo kuhatarisha ubora huduma za AZISE/AZAKI
- Tutahakikisha kunakuwepo na kutekelezwa kwa sera na taratibu zinazozuia mgongano wa maslahi, upendeleo na ufisadi

MAWASILIANO NA UPEANAJI TAARIFA

- Tunatambua umuhimu na nguvu ya mawasiliano na hivyo tutahakikisha kuwa nyenzo hii muhimu inatumika kwa uhakika na kwa wakati muafaka na wadau wote muhimu wa sekta.
- Tutahakikisha kunakuwepo na mifumo iliyowazi na ya uhakika ya usimamizi na utoaji taarifa

USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA KANUNI ZA MAADILI

- AZISE/AZAKI kwa ujumla wao au binafsi zinawajibikaji kusimamia, kufuatilia mienendo yao kimaadili na jinsi zinavyotekeleza maadili haya. Taarifa za matokeo ya ufuatiliaji wa utekelezaji maadili haya zitatolewa kwa wadau kupitia mikutano mikuu ya mwaka ya AZAKI/AZISE
- Kutaundwa Kamati za Ufuatiliaji katika ngazi za wilaya, mikoa au kutumia mitandao ya AZISE/AZAKI iliyopo katika wilaya kwa kadri ya makubaliano ya AZISE/AZAKI husika.
- Mitandao au Mashirika Miamvuli iliyopo au itakayoundwa baadaye itahakikisha kuwa wanachama wao wafuata nakutekeleza kanuni za maadili haya.
- Kutokubaliana au migogoro itakayotokana na utekelezaji wa Kanuni hizi kwa kiasi kikubwa itashughulikiwa na kamati au mtandao husika katika wilaya/ mkoa kwa kutumia taratibu na kanuni zilizopo na ikishindikana katika ngazi hiyo rufaa zitapelekwa ngazi ya juu ikiwa ni pamoja na Baraza la AZISE